

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

07 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 07 MEI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

205. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI
KAJAGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukitumia kikamilifu Kitengo cha Kukuza Tija kilichopo Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuhakikisha utekelezaji wa miradi mikubwa nchini unakuwa wa tija na kuwanufaisha Watanzania.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

206. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuajiri Wafamasia angalau katika kila Kituo cha Afya nchini ili kuimarisha usimamizi na mtiririko wa upatikanaji dawa.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

207. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza kingo za korongo linalopita katikati ya Mji wa Mpwapwa lisiendelee kutanuka ili kunusuru maisha na makazi ya Wananchi wa maeneo hayo.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**208. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA
KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara za Nyololo – Mtwango – Mafinga hadi Mgololo.

**209. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY
HHAYUMA (HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Kondoza – Gisambalang – Nangwa kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**210. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD
NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo Kikuu cha Taifa Kusini mwa Tanzania na Kanda nyingine ambazo hazina Vyuo Vikuu.

WIZARA YA KILIMO:

211. MHESHIMIWA ESTER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-
Ununuzi wa zao la pamba utaanza Mwezi Mei au Julai;-

Je, Serikali inatarajia kuwalipa Wakulima watakaouza Pamba kwa utaratibu gani kabla ya kuanza kwa ununuzi wa zao hilo ifikapo Mwezi Mei – Julai, 2021.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

212. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa bidhaa ya Kimataifa ili kuendeleza na kukuza Utamaduni wetu Duniani.

WIZARA YA NISHATI:

**213. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP
MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Vijiji na Vitongoji nchini ambavyo havijapatiwa umeme vitapatiwa huduma hiyo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**214. MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, nini kimepelekea mkwamo wa mkakati wa ujenzi wa Mji mpya wa Kawe kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na lini mradi huo utaendelea.


III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



(Majadiliano yanaendelea)



DODOMA
07 MEI, 2021

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE